
# Ukaguzi wa shule unaposhindwa kuwa na mafanikio:
## Dondoo Kutoka ukaguzi wa utendaji wa Programu ya Ukaguzi Shule za Sekondari Tanzania


## 1. Utangulizi

Ukaguzi wa shule ni nyenzo muhimu ya serikali, na hasa Wizara ya Elimu, ambayo inaweza kuitumia kuhakikisha utendaji mashuleni unaboreshwa. Hata hivyo, mafanikio yake yanategemea namna ukaguzi unavyofanyika, na iwapo matokeo ya ukaguzi yanatumiwa kama nyenzo ya kuchagiza maboresho ya utendaji wa shule. Kama ukaguzi haufanyiki kikamilifu, kama mawasiliano na mfumo mzuri wa kuwasilisha maoni vinakosekana, kama hakuna ufuatiliaji wa mapendekezo ya maboresho, na hakuna namna ya kutathmini iwapo ukaguzi unatekeleza wajibu na kuleta tija au la, kazi ya ukaguzi wa shule inaweza kuwa ni kama kupoteza tu muda na mali ya umma.

Kutokana na kiwango kikubwa cha wanafunzi wa sekondari kuendelea kufeli/kushindwa katika masomo ya msingi, hasa ya sayansi na hisabati, Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali hivi karibuni (mwaka 2008) ilifanya ukaguzi wa utendaji wa programu ya ukaguzi wa shule za sekondari[1]. Ukaguzi, ulilenga shughuli za ukaguzi wa shule zilizofanyika kati ya mwaka 2004 na 2006. Ulilenga kupima iwapo programu ya ukaguzi wa shule inatimiza vilivyo azma yake ya kulinda ubora stahiki wa mafunzo, na iwapo inashughulikia tatizo la wanafunzi wanaofanya vibaya katika shule za sekondari.

Muhtasari huu unawasilisha dondoo kutoka ukaguzi huu. Unaonesha kuwa programu ya ukaguzi wa shule haifanyi kazi yake kikamilifu na hivyo inashindwa kulinda ubora wa ufundishaji na maboresho yake kutokana na:

[1]Ripoti nzima inaweza kupatikana hapa www.nao.go.tz

Muhtasari huu umeandaliwa na Uwazi iliyopo Twaweza/Hivos Tanzania.

Uwazi, S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu +255 22 266 4301. Nukushi +255 22 266 4308.
Barua pepe: info@uwazi.org. Tovuti: www.uwazi.org.

- Kushindwa kutoa kipaumbele kwa masuala yanayohusu utendaji mbovu wa wanafunzi katika mchakato mzima wa ukaguzi,
- Kushindwa kutoa/kuwasilisha taarifa kikamilifu na kutofuatilia utekelezaji wa mapendekezo,
- Kushindwa kufuatilia na kusimamia ufanisi wa kaguzi za shule


Kutokana na hali hii, ukaguzi unashauri kwamba:
- Utendaji wa shule na wa wanafunzi kwenye mitihani upewe kipaumbele katika ukaguzi wa shule;
- Matokeo ya ukaguzi na mapendekezo yatolewe kwa utaratibu mzuri zaidi na kwa jamii pana zaidi, ili yafahamike kwa wazazi na umma kwa ujumla;
- Idara ya ukaguzi ya Wizara ya Elimu ipewe rasilimali na wafanyakazi wa kutosha kutekeleza jukumu lao, na,
- Wizara ya Elimu ianzishe utaratibu wa kufuatilia ufanisi wa program ya ukaguzi wa shule.

## 2. Mapungufu yako wapi?

### (i) Wanafunzi wengi zaidi wanashindwa katika masomo ya hisabati na sayansi licha ya ukaguzi

Mfumo wa elimu wa Tanzania unakabiliwa na changamoto kubwa ya kuhakikisha elimu bora inatolewa ili kuweka msingi mzuri wa rasilimali watu wenye uwezo. Hili linaonekana kwenye utendaji mbaya wa wanafunzi kwenye mitihani, na hasa katika masomo ya hisabati na sayansi. Kwa mujibu wa tathmini iliyofanywa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwenye programu ya ukaguzi wa Shule za Sekondari, asilimia 70 ya wanafunzi waliofanya mtihani wa kumaliza Elimu ya Sekondari mwaka 2004 walishindwa somo la hisabati. Idadi kubwa ya wanafunzi pia walishindwa masomo ya sayansi (mchoro 1). Kushindwa huko ni hasara kwa wanafunzi wenyewe, ambao uwezo wao wa kuendelea na masomo ya elimu ya juu unakua umevurugwa, na kwa taifa, ambalo uwezo wake wa kufikia malengo ya maendeleo unaathiriwa vibaya kwa namna zote ( moja kwa moja na kwa njia nyingine).

**Mchoro 1: Asilimia ya wanafunzi walioshindwa masomo ya hisabati na Sayansi**




**Chanzo cha data:** Matokeo ya mwaka 2004 kwa-masomo: Tathmini yautendaji wa program ya ukaguzi wa Shule za Sekondari, 2008; 2008-2009 Matokeo kila somo: Baraza la Mitihani la Taifa, takwimu za matokeo ya Mitihani.

Ingawa ukaguzi wa shule unafanyika kila mwaka, takwimu za hivi karibuni zilizotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa zinaonesha kuwa mwenendo wa wanafunzi wengi kushindwa kwenye mitihani unaendelea kuwa mbaya zaidi siku hadi siku. Mwaka 2009 karibu asilimia 82 ya wanafunzi waliofanya mtihani wa kumaliza kidato cha nne walishindwa somo la hisabati; hili ni ongezeko la kufeli la asilimia 12 zaidi kuliko wastani wa walioshindwa miaka mitano iliyopita.

Wanafunzi wengi zaidi pia walifeli kwenye masomo mengine ya sayansi mwaka 2009. Mwenendo huu unaonesha kwamba haiwezi kuchukuliwa kiurahisi tu kuwa kufanya ukaguzi kutaboresha matokeo ya shule na wanafunzi. Mkaguzi mkuu anaonesha kuwa, namna ukaguzi unavyofanywa, masuala yanayokaguliwa, namna taarifa za matokeo ya ukaguzi zinavyotolewa na kutumika, na namna utekelezaji unavyofuatiliwa na kutathiminiwa vyote ni muhimu. Hata hivyo, kuna mapungufu katika maeneo yote haya ambayo yanaweza kuwa yanachangia mwenendo mbaya wa viwango vya ufaulu.

### (ii) Sio shule zote zinakaguliwa kila mwaka kama kanuni zinavyoelekeza

Ukaguzi wa shule unafanywa ili kufuatilia na kusimamia utoaji elimu na kuangalia iwapo shule zinafuata mitaala iliyoidhinishwa na viwango vilivyowekwa ili kulinda ubora. Kuna aina tatu za kaguzi ambazo zinaweza kufanywa:

- Ukaguzi wa shule nzima: unagusa nyanja zote zinazohusu shule kama sehemu ya kujifunzia kwa kuzingatia mpango wa maendeleo ya shule;
- Ukaguzi maalum: unagusa nyanja/suala maalumu lenye tatizo, kama kwa mfano, kukiwa na tuhuma za kasoro katika usimamizi wa rasilimali, utovu wa nidhamu shuleni, au kuendelea kwa utendaji mbaya (kufeli) kwa wanafunzi; na,
- Ukaguzi wa kufuatilia: unafanywa baada ya ukaguzi mkuu au ukaguzi maalumu ili kuona nini kimebadilika.

Ukaguzi wa shule nzima unapaswa kufanyika mara moja kila mwaka. Hata hivyo, kwa mujibu wa Idara ya Ukaguzi wa Shule katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kutokana na uhaba wa wafanyakazi, usafiri, eneo la ofisi, vifaa na nyumba, shule inakaguliwa mara moja kwa miaka miwili. Kwa namna hiyo, kama **jedwali 1** linavyooonesha, ukiacha mwaka 2007/08, ni kaguzi chache sana zimekuwa zikifanyika kila mwaka tangu mwaka 2004/05. Mwaka 2008/09 ni asilimia 9 tu ya shule zilizokuwepo ndizo zilikaguliwa.

**Jedwali 1: Ukaguzi wa Shule za Sekondari mwaka 2004/05-2008/09**

| Mwaka | Shule zilizokuwepo | Shule zilizokaguliwa | |
|---|---|---|---|
| | | Idadi | asilimia |
| 2004/05 | 1734 | 406 | 23 |
| 2005/06 | 2063 | 785 | 38 |
| 2006/07 | 2567 | 678 | 26 |
| 2007/08 | 3485 | 1880 | 54 |
| 2008/09 | 3798 | 346 | 9 |

**Chanzo cha data:** Tathmini ya utendaji wa Programu ya Ukaguzi wa Shule za Sekondari mwaka 2004/05-2006/07: Hotuba za bajeti za Wizara ya Elimu 2008; 2007/08-2008/09

### (iii) Suala la utendaji mbaya wa wanafunzi kwenye masomo ya msingi halipewi kipaumbele cha juu kwenye mipango ya kaguzi

Mwongozo wa ukaguzi umeeleza hatua ambazo idara ya ukaguzi wa shule inapaswa kufuata wakati wa kupanga ukaguzi wake na vipengele vinavyohitaji kugusiwa wakati wa ukaguzi. Kwa mujibu wa kitabu

hicho cha mwongozo kwa wakaguzi, mpango wa ukaguzi unapaswa kuweka vipaumbele kwa kurejea masuala kama, shule zenye ufaulu duni kwenye mitihani ya mwisho, shule ambazo hazijakaguliwa kwa muda mrefu, namna ya kuzifikia, maombi ya ukaguzi, matatizo yaliyopo, misimu muafaka, (kwa kuangalia eneo ilipo shule kijiografia), mitihani, sikukuu za taifa na matukio mengine.

Licha ya kutajwa umuhimu wa kuzifikia (kuzikagua) shule zenye utendaji mbaya kwenye mitihani ya mwisho, ukaguzi umegundua kuna ushahidi mdogo sana unaoonesha kuwa suala hili linapewa umuhimu unaostahili kwenye mwongozo na nyaraka za mipango. Kwa kuzingatia mapitio ya vipengele 148 ambavyo kitabu cha mwongozo wa ukaguzi kinataka vikaguliwe, tathmini ya Mkaguzi Mkuu inaonesha kuwa hakuna kipengele hata kimoja kinacholenga moja kwa moja utendaji mbaya wa wanafunzi, na kwamba suala hili limegusiwa, kwa namna isiyo ya moja kwa moja, kupitia vipengele 16 tu kati ya 148 ambavyo kitabu cha mwongozo kinataka vifanyiwe ukaguzi.

**Jedwali 2: Masuala yanayohusiana na utendaji mbaya wa wanafunzi kwenye kitabu cha mwongozo wa ukaguzi wa shule.**

| **vipengele** | **Idadi ya masuala** | **Asilimia ya masuala** |
|---|---|---|
| Kipengele kinacholenga suala la utendaji mbaya wa wanafunzi moja kwa moja | 0 | 0 |
| Vipengele vinavyohusiana na wanafunzi wanaofanya vibaya katika mitihani (lakini si moja kwa moja) | 16 | 11 |
| Vipengele visivyohusiana kabisa na wanafunzi wanaofanya vibaya | 132 | 89 |
| Jumla ya vipengele ambavyo wakaguzi wanahitaji kuvipitia wakati wa ukaguzi | 148 | 100 |

**Chanzo cha data:** Ukaguzi wa Hesabu wa utendaji wa Programu ya Ukaguzi wa Shule za Sekondari, 2008.

Uchunguzi wa kina wa nyaraka nyingine za mipango uliofanywa na timu ya ukaguzi unaonesha pia kwamba, kuna ushahidi mdogo iwapo vipaumbele bayana vinawekwa katika mipango ya jumla ya ukaguzi kushughulikia kwa umakini tatizo la shule na wanafunzi wanaofanya vibaya kwenye somo lolote.

Mara nyingi mipango ya uendeshaji haioneshi kama masuala ya ufundishaji na ufaulu wa wanafunzi yatagusiwa kwenye ukaguzi wa shule. Lakini, badala yake mipango inakuwa inalenga kwenye idadi ya shule zitakazokaguliwa. Ukaguzi umegundua kuwa upungufu huu unajitokeza kwenye ngazi zote (ngazi ya taifa, kikanda, na vilevile ngazi ya wilaya) na unaathiri aina zote za ukaguzi (ukaguzi mkuu/wa shule nzima, ukaguzi wa ufuatiliaji na ukaguzi maalumu wa shule).

### (iv) Kaguzi hazishughulikii vya kutosha tatizo la wanafunzi wanaofanya vibaya

Athari za upungufu huu kwenye kitabu cha mwongozo wa ukaguzi inaonekana pia kwenye mwenendo halisi wa ukaguzi mkuu (wa shule nzima) na ukaguzi maalumu wa shule. Kwa mfano, kwa kuzingatia uchunguzi wa kina wa sampuli ya kaguzi 110 za shule nzima zilizofanyika kati ya mwaka 2004 na 2006, tathmini ya utendaji iligundua kuwa hakuna ripoti hata moja iliyochunguza kikamilifu tatizo la udondokaji (kuacha shule) wa wanafunzi, mfumo wa ufundishaji na ufaulu wa wanafunzi. Vile vile, ni ripoti chache sana zimeyataja masuala haya. Kwa mfano, ukaguzi umebaini kuwa asilimia 6 ya kaguzi zilizofanywa zimezungumzia kitu kuhusu hitaji la mafunzo ya ziada ya wanafunzi na ni asilimia 19 tu zimegusia suala la ufanisi wa ufundishaji (Jedwali 3).


**Jedwali 3: Kiwango ambacho masuala ya lazima ya wanafunzi wanaofanya vibaya kililengwa kugusiwa kwenye ukaguzi wa shule zima (% ya masuala yaliyokaguliwa)**

| | Ilichunguzwa kwa kina | Ilichunguzwa kidogo | ilitajwa | Haikuoneshwa kabisa |
|---|---|---|---|---|
| Kupambana na udondokaji | 0 | 2 | 3 | 95 |
| Ufanisi wa ufundishaji | 0 | 19 | 2 | 79 |
| Mafunzo ya ziada | 0 | 6 | 1 | 93 |
| Utendaji wa wanafunzi | 0 | 15 | 11 | 74 |

**Chanzo cha data:** Ukaguzi wa CAG wa utendaji kwenye Programu ya Ukaguzi wa Shule za Sekondari.

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa tatizo hili kwenye kaguzi maalumu na kaguzi za ufuatiliaji zilizofanyika kati ya miaka ya 2004 na 2007. Kati ya mwaka 2004 na 2005, idara ilifanya kaguzi maalumu 428 na karibu kaguzi 2,600 zaidi zilifanyika kati ya mwaka 2006 na 2007. Hakuna hata ukaguzi mmoja kati ya kaguzi maalumu zilizofanyika kati ya mwaka 2004 na 2005 uliogusia suala la utendaji mbaya wa wanafunzi(kufeli kwa wanafunzi) kama kipengele cha kipaumbele cha kuchunguzwa. Vilevile uchunguzi wa sampuli 91 za ripoti za ukaguzi wa shule kutoka kwenye orodha ya kaguzi zilizofanyika kati ya mwaka 2006 na 2007 hautoi ushahidi wowote unaoonesha kuwa kujifunza na utendaji wa wanafunzi uligusiwa kama suala la msingi katika ukaguzi maalumu.

**Mchoro 2: Masuala yaliyochunguzwa kwenye ukaguzi maalumu 2004-2007**




**Chanzo cha data:** Ukaguzi wa CAG wa utendaji kwenye Programu ya Ukaguzi wa Shule za Sekondari.

Inaonekana kuwa idadi kubwa ya kaguzi maalumu kipindi hiki ilipata msukumo kutokana na tuhuma za ubadhirifu/kasoro kwenye matumizi ya rasilimali, haja ya kukagua ujenzi wa majengo na mahitaji mengine yanahohusiana nayo, na tuhuma za utovu wa nidhamu wa walimu na/wanafunzi.

### (v) Taarifa zinazotokana na ukaguzi haziwasilishwi kikamilifu

Ukaguzi wa shule unazalisha taarifa muhimu kuhusu hali ya elimu na changamoto za kipekee zinazo-athiri ufundishaji na ufanisi wa kujifunza shuleni. Namna ambavyo taarifa hizi hutolewa na kutumika kama nyenzo ya mabadiliko na maendeleo ni kitu cha muhimu sana. Kwa mujibu wa tathmini ya utendaji wa programu ya ukaguzi, idara ya ukaguzi haizuiliwi kuyawasilisha matokeo ya ukaguzi kwa umma wa wananchi. Na kwa kweli, sera inapendelea taarifa zijulikane kwa umma.

Kutokana na ukweli huu, ingetarajiwa kwamba idara ya ukaguzi ingewasilisha matokeo yake kutoka kwenye kaguzi sio tu kwa maafisa wa serikali[2], lakini pia kwa walimu wakuu wa shule zilizokaguliwa, kwa bodi za shule na kwa wazazi kupitia bodi za shule. Taarifa pia zinapaswa kutolewa kwa umma wa wananchi kupitia vyombo vya habari, na kupitia machapisho, kwa mfano, vijitabu, vijarida na njia za kielektroniki, mathalani kupitia tovuti ya Wizara ya Elimu.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa ingawa ripoti za ukaguzi zinasambazwa kwa wawakilishi wa serikali pamoja na mamlaka za serikali za mitaa na wadau wengine, namna zinavyowasilishwa haileti tija na ubora wa mawasiliano pamoja na matumizi mazuri ya matokeo ya kaguzi. Kwa mfano:

- Hakuna utaratibu ulioimarika wa kuhakikisha ripoti za ukaguzi wa shule zinatumwa kwenda kwenye ngazi ya tawala za wilaya pindi zinapokamilika,
- Wakati idara ya ukaguzi inatakiwa kuweka kumbukumbu zilizosainiwa zinazohusu majadiliano yaliyofanywa kati ya wakaguzi na menejimenti ya shule, kumbukumbu hizo hazikuweza kutolewa kwa wakaguzi waliotathmini utendaji kuonesha kwamba hilo linafanyika kiuhalisia.
- Kuna uwazi mdogo: taarifa zinazohusu ukaguzi hazichapishwi, hii inamaanisha kuwa hazipatikani kwa vyombo vya habari na kwa wananchi kwa ujumla. na,
- Hakuna tathimini inayofanywa kujua ni kwa namna gani na kwa kiwango gani taarifa zinazotokana na ukaguzi wa shule zimetumiwa ipasavyo na iwapo malengo yake yamefikiwa.

### vi) Mapendekezo kwenye ripoti za ukaguzi wa shule hayashughulikiwi ipasavyo

Ukaguzi wa shule unapaswa kusaidia na kuinua ubora wa utendaji wa shule na wanafunzi. Ili hili lifanyike, ripoti za ukaguzi zinatarajiwa kuwapatia walimu wakuu na/au menejimenti za shule mapendekezo muhimu na yanayotekelezeka ambayo yanaweza kutumika kusukuma mabadiliko. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kutokana na uchunguzi wa kina wa aina ya ushauri unaotolewa kwa menejimenti za shule, kuwa mapendekezo mengi hayakidhi vigezo, na hivyo kuna uwezekano yasiweze kuzinufaisha tawala kuboresha utendaji. Baadhi ya kasoro zilizobainika kwenye mapendekezo ni kwamba:

- Mapendekezo machache sana yalilenga suala la wanafunzi wanaofanya vibaya zaidi, namna ya kushughulikia udondokaji, na namna ya kuboresha ujifunzaji na ufundishaji shuleni na/au mapungufu ya mafunzo shuleni.
- Ushauri unaotolewa kwa shule mbali mbali huwa unafanana na unajirudia rudia kwa kipindi fulani kwa mwendelezo wa namna ileile bila kuonesha hoja za kuunga mkono mapendekezo hayo.

---

[2] Mkaguzi mkuu; Katibu Mkuu Wizara ya Elimu; mamlaka za Mitaa zinazohusika na shule (Afisa Tawala wa Wilaya, Maafisa Elimu wa Wilaya na Makatibu Tawala wa Mikoa)

- Katika baadhi ya maeneo mapendekezo yanayotokana na ukaguzi yanakuwa hayatekelezeki (yako nje ya uwezo wa shule husika) au yanahitaji rasilimali za ziada ambazo sio rahisi kwa shule kuzipata.

Ukaguzi wa utendaji ulibaini pia kuwa kwenye maeneo mengi mapendekezo yanayotolewa yanailenga Wizara ya Elimu japo hili halisemwi wazi, maana yanakwenda nje ya uwezo wa utawala wa shule kuyatekeleza. Kwa mfano, karibu asilimia 70 ya ripoti za ukaguzi, zilishauri shule ziongeze walimu zaidi; na asilimia 50 zilikuwa na ushauri wa kuhakikisha vitabu zaidi vinapatikana; na kwenye asilimia 65 ya kaguzi kulikuwa na ushauri wa kujenga au *kukarabati* majengo ya shule.

### (vii) Utaratibu/mfumo wa ufuatiliaji na kutathimini ufanisi wa ukaguzi haupo

Mkaguzi wa shule anahitaji kujua ni kwa kiwango gani jitihada na mapendekezo yake yamechangia kufikiwa malengo yake ya uboreshaji wa utendaji shuleni. Kwa hiyo, ukaguzi wa shule unapaswa kufuatiliwa na kutathiminiwa kama sehemu muhimu ya mchakato wa kujifunza kuhusu nini kimefanikiwa na nini kimeshindwa kuleta mafanikio, ili kuboresha ukaguzi wa siku zijazo. Ingawa aina fulani ya ufuatiliaji inaonekana kuwepo, ukaguzi wa utendaji umebaini kwamba shughuli zinazohusishwa hazijitoshelezi kama tathimini halisi.

Matokeo ni kwamba kuna ushahidi mdogo na usiotosha kuthibitisha kwamba mapendekezo yanayotolewa na ukaguzi wa shule yanatekelezwa kweli, na kama ni hivyo, athari zake ni zipi? Mathalan, timu ya wakaguzi walibainisha kwamba hawakuweza kupata nyaraka zozote za mkusanyo wa mapendekezo ya ukaguzi wa shule na viashiria vinavyoonesha iwapo mapendekezo hayo yalitekelezwa. Idara ya Ukaguzi wa shule pia haukuweza kuipatia Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi tathimini kamilifu ya:

- Mtazamo wa wadau kuhusu mapendekezo yaliyotolewa, na
- Matokeo yaliyopatikana kutokana na hatua zilizochukuliwa

## 3. Hitimisho na mapendekezo

Ukaguzi wa utendaji wa programu ya ukaguzi kwa shule za sekondari umeonesha kuwa kuna mapungufu kadhaa ambayo yanazuia uwezo wake kulinda kikamilifu ubora wa ujifunzaji/elimu na utendaji kwenye shule. Ukaguzi hasa unaonesha kwamba:

- Suala la utendaji mbaya wa wanafunzi katika mitihani halijapewa kipaumbele kinachostahili kwenye miongozo, mipango ya ukaguzi wa shule na kwenye shughuli za kikaguzi;
- Mapendekezo mara nyingi hayawalengi wahusika halisi na yana gharama kubwa mno kuyatekeleza, hivyo hayatekelezeki;
- Utendaji wa utaratibu wa mawasiliano na kutoa maoni kuhusu ukaguzi haufanyi kazi kikamilifu
- Usiri kuhusiana na taarifa za ukaguzi unafanya zisiweze kuwafikia wananchi na vyombo vya habari hata wakazichambua. Hii inamaanisha kuwa maoni ya jumla ya wananchi na michango yao katika kusukuma mabadiliko chanya hayachukuliwi; na,
- Kukosekana kwa utaratibu makini wa kusimamia ufanisi wa ukaguzi kuna maana kuwa ujenzi wa uelewa unaofanyika ndani ya programu ni hafifu.

Yote haya yanaashiria kwamba uwezo wa kaguzi za shule kuisaidia serikali katika kuandaa sera na mikakati ya kushughulikia utendaji usioridhisha ni dhaifu. Lakini, hili linaweza kushughulikiwa. Hivyo, ukaguzi wa utendaji unapendekeza kwa Idara ya Ukaguzi wa Shule, kuanza kuyafanyia kazi mapungufu

yaliyobainika. Na kwa Wizara ya Elimu, ihakikishe Idara ya Ukaguzi wa Shule ina wafanyakazi, vifaa na rasilimali za kutosha ili iweze kutekeleza wajibu wake kikamilifu.

## Rejea

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania(2008), Ripoti ya ukaguzi wa utendaji wa Programu ya Ukaguzi wa Shule za Sekondari nchini Tanzania, Dar es Salaam, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Tanzania

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania(2007, 2008), Hotuba za Bajeti za Wizara ya Elimu na Mfunzo ya Ufundi.